**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**
**WAKALA WA HUDUMA ZA MISITU TANZANIA**

# TANGAZO

## UUZAJI WA MAGOGO YA MTI WA MKURUNGU KWA NJIA YA MNADA KATIKA ENEO LA BANDARI YA NCHI KAVU – UBUNGO, DAR ES SALAAM

1. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) utauza magogo vipande 18,489 ya mti wa Mkurungu (*Pterocarpus Tinctorius*) yenye jumla ya meta za ujazo **1,357.026** iliyopo katika eneo la Bandari ya Nchi Kavu – Ubungo, Dar es Salaam.

2. Magogo hayo ya Mkurungu yamepimwa ujazo uliopo katika makasha 59 na yatauzwa kwa njia ya mnada kwa kuzingatia Kanuni ya 31 (ii) ya Kanuni za Sheria ya Misitu za Mwaka 2004. Magogo hayo yatauzwa mahali yalipohifadhiwa na jinsi yalivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo.

3. Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika eneo la **Bandari ya Nchi Kavu - Ubungo**. Mnada utafanyika siku ya **Jumatatu** ya tarehe **09 Agosti, 2021** kuanzia saa **4:30 asubuhi**.

4. Mnunuzi anakaribishwa kutembelea eneo la Bandari ya Nchi Kavu - Ubungo ili kukagua mazao hayo ya misitu muda wa kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) alasiri siku za Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu. Ukaguzi huo utafanyika kuanzia tarehe ya Tangazo hili hadi tarehe **08 Agosti, 2021**. Aidha, Maafisa Misitu wa Wakala watakuwepo kwa ajili ya kutoa maelezo ya ziada ikiwa yatahitajika.

5. Mnunuzi mwenye nia ya kushiriki mnada anatakiwa kuwasilisha kwenye bahasha iliyofungwa nia yake ya kushiriki mauzo akiainisha namba ya fungu na pendekezo la bei kwa meta moja ya ujazo anaotarajia kununua kwa kufuata majedwali namba 1 hadi 6 ya Tangazo hili. Aidha, majedwali haya yatatumika kuchagua fungu lenye magogo ya kununua kwa kuzingatia taarifa zilizoorodheshwa kama ifuatavyo: -

**JEDWALI Na. 1: ORODHA YA MAKASHA YENYE MAGOGO KATIKA FUNGU NAMBA 1 BANDARI YA NCHI KAVU – UBUNGO**

| Fungu Na. | Jina la Kasha | Idadi ya Magogo kwa kasha | Meta za ujazo kwa Fungu ($M^3$) | Bei ya kuanzia kwa kila meta za ujazo za kila fungu (TZS/$M^3$) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MRKU 4670133 | 360 | 289.175 | 1,167,568 |
| | MRKU 0470081 | 345 | | |
| | PONU 7529326 | 330 | | |
| | MRKU 0761976 | 277 | | |
| | TCNU 8495914 | 420 | | |
| | MRKU 4029963 | 343 | | |
| | PCIU 8910373 | 485 | | |
| | MSKU 9035410 | 465 | | |
| | MSKU 9574290 | 372 | | |
| | TGHU 7623118 | 431 | | |
| | **Jumla** | **3,828** | | |

**JEDWALI Na. 2: ORODHA YA MAKASHA YENYE MAGOGO KATIKA FUNGU NAMBA 2 BANDARI YA NCHI KAVU – UBUNGO**

| Fungu Na. | Jina la Kasha | Idadi ya Magogo kwa kasha | Meta za ujazo kwa Fungu ($M^3$) | Bei ya kuanzia kwa kila meta za ujazo za kila fungu (TZS/$M^3$) |
|---|---|---|---|---|
| 2 | MRKU 4392881 | 306 | 253.266 | 1,144,335 |
| | MRKU 4189046 | 234 | | |
| | MSKU 1555755 | 274 | | |
| | TGHU 9472406 | 376 | | |
| | MSKU 6260720 | 286 | | |
| | PCIU 8199774 | 279 | | |
| | TGHU 8691858 | 435 | | |
| | MSKU 6162750 | 344 | | |
| | MSKU 6966189 | 299 | | |
| | MIEU 0057381 | 273 | | |
| | **Jumla** | **3,106** | | |

## JEDWALI Na. 3: ORODHA YA MAKASHA YENYE MAGOGO KATIKA FUNGU NAMBA 3 BANDARI YA NCHI KAVU – UBUNGO

| Fungu Na. | Jina la Kasha | Idadi ya Magogo kwa kasha | Meta za ujazo kwa Fungu ($M^3$) | Bei ya kuanzia kwa kila meta za ujazo za kila fungu (TZS/$M^3$) |
|---|---|---|---|---|
| 3 | TCLU 5958026 | 449 | 241.071 | 1,194,545 |
| | BMOU 4384225 | 258 | | |
| | PCIU 8894122 | 440 | | |
| | CBHU 8497894 | 251 | | |
| | CMAU 5815607 | 282 | | |
| | PONU 7934524 | 312 | | |
| | MRKU 0498330 | 273 | | |
| | MRKU 2389791 | 238 | | |
| | GLDU 7462085 | 364 | | |
| | MSKU 8582963 | 484 | | |
| | **Jumla** | **3,351** | | |

## JEDWALI Na. 4: ORODHA YA MAKASHA YENYE MAGOGO KATIKA FUNGU NAMBA 4 BANDARI YA NCHI KAVU – UBUNGO

| Fungu Na. | Jina la Kasha | Idadi ya Magogo kwa kasha | Meta za ujazo kwa Fungu ($M^3$) | Bei ya kuanzia kwa kila meta za ujazo za kila fungu (TZS/$M^3$) |
|---|---|---|---|---|
| 4 | MAEU 6203471 | 288 | 224.659 | 1,206,728 |
| | PONU 1735037 | 341 | | |
| | TCNU 9256750 | 291 | | |
| | MRKU 4642487 | 254 | | |
| | MRKU 0882089 | 339 | | |
| | MSKU 1869709 | 288 | | |
| | INKU 2224640 | 263 | | |
| | TEMU 6485178 | 178 | | |
| | MSKU 6162679 | 327 | | |
| | MSKU 8710323 | 357 | | |
| | **Jumla** | **2,926** | | |

**JEDWALI Na. 5: ORODHA YA MAKASHA YENYE MAGOGO KATIKA FUNGU NAMBA 5 BANDARI YA NCHI KAVU – UBUNGO**

| Fungu Na. | Jina la Kasha | Idadi ya Magogo kwa kasha | Meta za ujazo kwa Fungu ($M^3$) | Bei ya kuanzia kwa kila meta za ujazo za kila fungu (TZS/$M^3$) |
|---|---|---|---|---|
| 5 | PCIU 8331520 | 297 | 206.470 | 1,222,465 |
| | PCIU 8574690 | 223 | | |
| | AAAU 4000216 | 264 | | |
| | TCLU 1482369 | 275 | | |
| | UESU 4122258 | 278 | | |
| | GESU 5044285 | 324 | | |
| | MSKU 6257481 | 254 | | |
| | TCKU 9652865 | 362 | | |
| | EISU 9386912 | 277 | | |
| | MRKU 5458915 | 528 | | |
| | **Jumla** | **3,082** | | |

**JEDWALI Na. 6: ORODHA YA MAKASHA YENYE MAGOGO KATIKA FUNGU NAMBA 6 BANDARI YA NCHI KAVU – UBUNGO**

| Fungu Na. | Jina la Kasha | Idadi ya Magogo kwa kasha | Meta za ujazo kwa Fungu ($M^3$) | Bei ya kuanzia kwa kila meta za ujazo za kila fungu (TZS/$M^3$) |
|---|---|---|---|---|
| 6 | MSKU 0516727 | 305 | 142.385 | 1,310,303 |
| | CLHU 8931911 | 197 | | |
| | MSKU 0129740 | 284 | | |
| | MRKU 3664012 | 241 | | |
| | MSKU 0377941 | 262 | | |
| | PONU 7389564 | 356 | | |
| | MRKU 2080930 | 262 | | |
| | PCIU 8027409 | 216 | | |
| | MSKU 8023815 | 73 | | |
| | **Jumla** | **2,196** | | |

6. Idadi ya magogo kwa kila fungu itanadiwa peke yake kulingana na bei na ujazo uliopo. Hata hivyo, bei ya juu itakayotolewa na mnunuzi mshiriki wakati wa kufungua bahasha ndiyo itakuwa bei ya kuanzia kunadi kila

meta moja ya ujazo kwa fungu na bei hiyo haitazuia wanunuzi wengine kuongeza bei zao wakati wa mnada.

7. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania utatoa barua ya ushindi kwa mnunuzi aliyeshinda mnada wa kila fungu.

8. Mnunuzi atakayeshinda atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25 %) ya thamani yote ya ununuzi siku ya mnada. Fedha hizo hazitarudishwa endapo mshindi atashindwa kulipia ujazo wote aliouziwa. Aidha, asilimia sabini na tano (75 %) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia siku ya mnada. Malipo yote yafanyike kupitia benki au mitandao ya watoa huduma za kifedha baada ya kupewa hati ya madai (bill) kutoka Mfumo wa Makusanyo ya Serikali (GePG) itakayotolewa na Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu (TFS).

9. Mnunuzi aliyeshinda atapaswa kuwasilisha hati ya malipo (pay-in-slip) kwa mkuu wa kitengo cha Leseni cha Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kama uthibitisho wa malipo na siyo zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.

10. Mnunuzi aliyeshinda mnada atatakiwa kuondoa mazao ya misitu aliyonunua ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya kumaliza kulipa malipo yote kwa asilimia 100. **Aidha, kibali cha kusafirisha magogo nje ya nchi kitatolewa kwa tangazo maalumu la Serikali (Government Notice) kwa kila Mshindi atakayehitaji kusafirisha magogo hayo nje ya nchi**.

11. Usajili wa wanunuzi na watazamaji wenye nia ya kushiriki mnada utafanyika katika eneo la Bandari ya Nchi Kavu - Ubungo kuanzia saa moja na nusu (1:30) asubuhi hadi saa nne kamili (4:00) asubuhi siku ya mnada. Aidha, wanunuzi watakaochelewa kuwasilisha nia zao kwa siku na muda uliopangwa hawataruhusiwa kushiriki katika mnada.

12. Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti zifuatazo za: www.tfs.go.tz na www.mnrt.go.tz.

Limetolewa na

**KAMISHNA WA UHIFADHI**
**S. L. P 40832**
**DAR ES SALAAM**